

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA**

**09 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 09 MEI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**264. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI  
MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imejipanga vipi kushughulikia malalamiko kuhusu Kikokotoo.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**265. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO  
KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Hospitali ya Halmashauri ya Mji Handeni.

**266. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS  
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamalizia Vituo vya Afya Kizengi, Tura, Lutende na Goweko kwa kujenga *OPD* na kupeleka Vifaa Tiba.

**267. MHESHIMIWA SAMWEL XADAY HHAYUMA  
(HANANG’):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya Mureru – Diloda – Gorimba – Masusu hadi Waama ili ipitike wakati wote.

**268. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD  
KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule ya Msingi ya Watoto wenye Mahitaji Maalum katika Halmashauri ya Morogoro.

**WIZARA YA KILIMO:**

**269. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA  
(NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kwa nini Skimu za Umwagiliaji za Liyuni na Limamu – Namtumbo hazikamiliki ingawa Serikali imetumia fedha nyingi.

**270. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE  
SAMIZI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Wakulima wa Tumbaku watalipwa fedha zao kutoka Kampuni ya JESPAN za msimu wa mauzo 2021 Jimboni Muhambwe.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **271. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga nyumba za Askari Polisi katika Kituo cha Wilaya ya Micheweni.

### **272. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza msongamano wa Wafungwa Magerezani.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **273. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Singida – Ilongero hadi Hydrom.



**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA  
BIASHARA:**

**274. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji,  
Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mpango gani kufanya utafiti na  
kurasimisha Pombe ya MWIKI inayotokana na  
mabibo ili kuongeza thamani ya zao la korosho.

**WIZARA YA MADINI:**

**275. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE  
WAITARA (TARIME VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Wananchi wa Komarera, Nyamichele na  
Murwambe katika maeneo ya Mgoji wa Barrick  
North Mara watalipwa fidia.

**276. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED  
KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali itafungua Ofisi ya Madini Liwale.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**277. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha  
kuwa Vyuo Vikuu vyenye Taaluma ya Sayansi  
na Tiba vinakuwa na Hospitali za kufundishia.

**WIZARA YA MAJI:**

**278. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA  
(MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakarabati miundombinu  
chakavu ya maji na kuhakikisha upatikanaji wa  
maji ya kutosha katika Mji wa Mbinga.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**279. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA  
(CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na  
Sheria:-

Je, lini hatua iliyobakia katika mchakato wa kupata Katiba Mpya itakamilishwa.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI WA KILIMO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
09 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**